**OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA**
**MPANGO WA MAFUNZO YA LUGHA YA KIINGEREZA (DSS-6233)**

**UTATHMINI WA HUDUMA:**

1. Jina ______________________________________________

2. Hati ya Kustahiki Imeambatishwa: NDIYO ☐ HAPANA ☐ 3. Jinsia: Mwanamume ☐ Mwanamke ☐
4. Nambari ya Mgeni: ______________________________

5. Tarehe ya Kuwasili: _______________ 6. Tarehe ya kuzaliwa: _______________ 7. Hali ya Uhamiaji: ______________________

8. Anwani: ________________________________________ 9. Nambari ya Simu: __________________________

______________________________________10. Anwani ya Barua Pepe: ___________________________________

11. Nchi ya Asili: _________________12. Lugha ya Msingi: ________________ 13. Lugha Nyingine/Zingine: ___________________

14. Usafiri Unahitajika: NDIYO ☐ HAPANA ☐ 15. Mipango ya Sasa ya Usafiri, ikiwa ipo: _______________________________

16. Historia ya Elimu/Kazi: ______________________________________________

17. Ratiba ya Kazi: _________________________________18. Huduma ya Matunzo ya Watoto: _______________________________

**MPANGO WA HUDUMA:**

| | | A | B* | C | D | E |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MSIMBO** | **HUDUMA** | **Ndiyo/ Hapana** | **Sababu** | **Tarehe ya Kuanza kwa Huduma** | **Maoni ya Rufaa** | **Herufi za Kwanza za Jina la Mteja** |
| 923 | Usafiri | | | | | |
| 927 | ELT-Kiwango cha Juu | | | | | |
| 928 | ELT-Kiwango cha Msingi | | | | | |
| 929 | ELT-Kiwango cha Kati | | | | | |
| 930 | Mafunzo ya Lugha ya Kiingereza | | | | | |
| 931 | ELT (Rufaa ya ELT) | | | | | |
| 955 | Maelezo na Rufaa | | | | | |
| 961 | Mafunzo ya Raia wa Marekani na Mafunzo ya Raia ya Lugha ya Kiingereza | | | | | |
| 965 | Tafsiri na Ukalimani | | | | | |

Eleza lengo/malengo ya ELT ya mteja na hatua za kuchukuliwa ili kufanikisha lengo hilo. Jumuisha ustadi wa Kiingereza na mafunzo yoyote ya awali.

______________________________________________

______________________________________________

*Mimi, ________________________________________, ninakubali mpango wa ELT kama nilivyoelezewa. Ikiwa nina maswali yoyote au ninahitaji maelezo ya ziada, ninaweza kuwasiliana na Mfanyakazi wa ELT kwa nambari iliyowekwa hapa chini.*

Saini ya Mteja: _____________________________________Tarehe: ____________________________

Saini ya Mkalimani: _________________________________ Tarehe: ____________________________

Jina la Mfanyakazi wa Shirika la ELT: ______________________________ Nambari ya Simu: ______________________

Anwani ya Barua Pepe: _______________________________ Tarehe: ____________________________

Je, unabadilisha mtihani wa ESL ulioidhinishwa Idara ya Vyuo vya Jamii ya NC (Department of Community Colleges), kama vile CASAS au BEST?

NDIYO ☐ Tafadhali andika tarehe ya mtihani na alama hapa **au** ambatisha mtihani uliokamilishwa kwenye fomu hii ili ujumuishwe kwenye faili.

Tarehe ya Mtihani: ______________________ Alama: _______________

HAPANA [ ] Tafadhali endelea kujaza Fomu ya Mtihani wa Kwanza wa ELT ya DSS-6234 na ujumuishe kwenye faili.

**Katika Miezi 3/Miezi 6/Miezi 12:** Tumia Fomu ya Ukaguzi wa Mpango (DSS-6235)

**Maagizo ya Kujaza Fomu ya**
***Mpango wa Huduma ya Mafunzo ya Lugha ya Kiingereza (DSS-6233) ya Ofisi ya Wakimbizi ya Jimbo la NC***

**Madhumuni**: Madhumuni ya Mpango wa Huduma ya ELT ni kutoa zana ambayo shirika na mteja, kwa pamoja, watatathmini na kukagua ujuzi, uwezo na maslahi ya mteja ili kubaini huduma za ELT zinazofaa kutolewa. Mpango huo unapaswa kujumuishwa kwenye faili ya mteja **pamoja na Fomu ya Idhini ya Ufahamu ya Kutolewa kwa Maelezo (DSS-6236) na Fomu ya Haki za Mteja (DSS-6237)** katika kituo cha mtoa huduma wa eneo au kituo cha mtoa huduma za wakimbizi. **Fomu ya Mtihani wa Kwanza wa ELT ya DSS-6234** inapaswa pia kujumuishwa, ikiwa inatumika. Mpango wa ELT LAZIMA uundwe kwa kila mteja anayepokea huduma za ELT za moja kwa moja.

**UTATHMINI WA HUDUMA:**

1. Jina: Andika jina la mteja binafsi ambaye anaundiwa Mpango wa Huduma ya ELT.

2. Hati ya Kustahiki: Tia alama kwenye kisanduku kinachofaa ili kuonyesha iwapo hati za ustahiki zilitolewa wakati wa kuundwa kwa Mpango wa Huduma ya ELT. KUMBUKA: Huduma haziwezi kuanza kutolewa hadi mteja awasilishe hati zinazofaa ili kuthibitisha kwamba anastahili kushiriki katika Huduma za Mpango wa Wakimbizi. **Mtu anayejaza mpango huu lazima aambatishe/ajumuishe nakala ya sasa ya hati ya kustahiki kwenye mpango wa huduma siku ya kujazwa kwa fomu.**

3. Jinsia: Tia alama ya tiki kwenye kisanduku kinachofaa ili kuonyesha jinsia ya mteja.

4. Nambari ya Mgeni: Weka Nambari ya Mgeni ya mteja.

5. Tarehe ya Kuwasili: Weka tarehe rasmi ya kuwasili kwa mteja, kama ilivyoorodheshwa kwenye I-94, Cheti cha Kuomba Makao au hati zingine zinazofaa.

6. Tarehe ya kuzaliwa: Weka tarehe ya kuzaliwa ya mteja.

7. Hali ya Uhamiaji: Weka hali ya **sasa** ya mteja (Mkimbizi, Mtafuta Hifadhi, Mfungwa Anayehudumia Kifungo cha Nje, Mkuba/Mhaiti Mgeni, Mtu Mwenye Asili Mchanganyiko wa Maerkani na Asia, Mkazi wa Halali wa Kudumu, Mwathirika wa Ulanguzi wa Watu, SIV, nk).

8. Anwani: Weka anwani ya nyumbani, ikiwa ni pamoja na jiji, jimbo na msimbo wa eneo, wa mteja.

9. Simu: Weka nambari ya simu ya nyumbani na/au nambari ya simu ya mkononi ya mteja.

10. Barua Pepe: Weka anwani ya barua pepe ya mteja, ikiwa inatumika.

11. Nchi ya Asili: Weka nchi ya asili ya mteja.

12. Lugha ya/za Msingi: Weka lugha ya msingi (ya asili) ya mteja ambayo alizungumza katika nchi yake ya asili.

13. Lugha Nyingine: Weka lugha zingine zozote ambazo mteja anaweza kusoma, kuandika au kuzungumza.

14. Usafiri Unahitajika: Tia alama kwenye kisanduku kinachofaa ili kuonyesha iwapo mteja atahitaji msaada wa usafiri ili kuweza kwenda kupata huduma zinazohitajika.

15. Mipango ya: Usafiri: Weka maelezo muhimu kuhusu mpango wa usafiri wa mteja.

16. Historia ya Elimu/ Kazi: Jumuisha maelezo yoyote muhimu kuhusu historia ya elimu au kazi ya mteja.

17. Ratiba ya Kazi: Weka maelezo yoyote kuhusu ratiba ya sasa ya kazi ya mteja, ikiwa inafaa.

18. Huduma ya Matunzo ya Watoto: Weka maelezo muhimu kuhusu mpango wa mteja unaohusiana na huduma ya matunzo ya watoto, ikiwa inafaa.

**MPANGO WA HUDUMA:**

**Safuwima ya A:** Onyesha huduma zinazoombwa na mteja au zinazotolewa kwa mteja.
**Safuwima ya B:** Ikiwa uamuzi wa mratibu wa mpango wa mteja ni kumkataza mteja huduma, onyesha nambari ya sababu kutoka kwa sababu zilizoorodheshwa katika sehemu ya kabla ya kupangilia ya Mpango wa Huduma.
**Safuwima ya C:** Ikiwa huduma zitatolewa, onyesha tarehe ya kuanza kwa huduma kwenye safuwima hii.
**Safuwima ya D:** Ikiwa rufaa zinafaa, weka maoni kuhusu mtoa huduma au shirika ambalo mteja ataelekezwa ili kupata huduma.
**Safuwima ya E:** Mteja anapaswa kuweka herufi za kwanza za jina la kila huduma katika safu hii ili kuonyesha kwamba anaelewa kila huduma inayotolewa au aliyonyimwa, na amepewa huduma inayofaa au anaelewa sababu ya kunyimwa huduma. Tumia nafasi iliyo chini ya jedwali kwa maelezo yoyote ya ziada.
**KUMBUKA: Ikiwa mteja ataomba huduma yoyote ya ajira, shirika linapaswa kujaza mpango wa uwezo wa kuajiriwa kwa mteja.**

**Misimbo ya Sababu za Kunyimwa/Kucheleweshwa kwa Huduma:**

01 Huduma haipatikani kupitia mtoa huduma
02 Huduma haipatikani kwa sasa; itapatikana kufikia ____________
03 Mteja lazima awasilishe hati zinazofaa kabla ya huduma kuanza
04 Mteja anastahili kupookea huduma lakini fedha hazipatikani
05 Huduma haipatikani katika eneo ambalo mteja anaishi
06 Mteja hastahili kupokea huduma aliyoombwa
07 Huduma hiyo ilitolewa awali kwa mteja
08 Kurudiwa kwa huduma iliyopo
09 Mteja alikataa huduma hiyo

**SAINI:**

Andika jina la mteja katika nafasi iliyowekwa ambayo inaonyesha kuwa mteja anaelewa Mpango wa Huduma ya ELT.

Saini ya Mteja: Hakikisha mteja anatia saini Mpango wa Huduma baada ya kufafanuliwa na kutafsiriwa.

Tarehe: Weka tarehe ambayo mteja anatia saini Mpango wa Huduma.

Jina la Mkalimani: Andika jina la mkalimani au mfanyakazi aliyemtafsiria mteja wakati wa kuundwa kwa Mpango wa Huduma ya ELT. Ikiwa hakuna mkalimani aliyehitajika, tafadhali andika Haitumiki.

Saini ya Mkalimani: Hakikisha mkalimani anatia saini Mpango wa Huduma baada ya kufafanuliwa na kutafsiriwa.

Tarehe: Weka tarehe ambayo mkalimani anatia saini Mpango wa Huduma.

Mfanyakazi wa Shirika: Andika jina la mfanyakazi aliyejaza fomu na mteja.

Nambari ya Simu: Weka nambari ya simu inayoweza kutumiwa kuwasiliana na mfanyakazi wakati wa saa za kawaida za kazi.

Anwani ya barua pepe: Weka anwani ya barua pepe ya mfanyakazi.

Tarehe: Weka tarehe ambayo mfanyakazi anatia saini Mpango wa Huduma ya ELT.

**UNABADILISHA?**

Tia alama kwenye kisanduku kinachofaa ikiwa unabadilisha mtihani unaokubalika, kama vile CASAS au BEST, badala ya Fomu ya Mtihani wa Kwanza wa Wanafunzi wa ELT ya DSS-6234. Jumuisha matokeo ya mtihani katika nafasi iliyowekwa na uambatishe na ujumuishe kwenye faili ya mteja. Ikiwa hubadilishi, tafadhali endelea na Mtihani.